

Handeni Yetu



Halmashauri ya Wilaya ya Handeni.

Octoba- Desemba 2016 Toleo Namba 02

HUTOLEWA KILA BAADA YA MIEZI MITATU



Mkuu wa Wilaya azin-
dua umezaji
dawa
uk 4

Waziri Jafo awaasa
watumishi wa umma
Handeni .
Uk 6



Habari
Katika
Picha
Uk
11&12



Mkuu wa Wilaya Bw.Gondwe awataka watumishi kusimamia misingi ya utawala bora Uk 5



YALIYOMO NDANI

Maadhimisho ya siku ya maadili na haki za binadamu yafanyik kiwilaya Uk 9



vibakuli 500 na mbao 914 za mkarambati zakamatwa Uk 04



Mkuu wa Wilaya Bw. Godwin Gondwe akizungumza na watumishi na Viongozi kwenye kikako cha Utawala bora katika ukumbi wa Anglikana Handeni.

Kamati ya Fedha ,Uongozi na Mipango imefanya ziara ya kukagua miradi ya maendeleo ya MIVARF na SEDP II

Kamati ya Fedha ,Uongozi na Mipango kwa kuongozwa na mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni Bw. Ramadhani Diliwa na Mwenyekiti wa FUM wamefanya ziara ya kutembelea Miradi ya maendeleo ambayo ipo chini ya MIVARF na SEDP II.

Ukaguzi huo umefanywa ili kujiridhisha na maendeleo lakini pia

kuona mlingano wa thamani ya fedha na shughuli inayofanywa(value for money).

Mapungufu yalibainishwa na waheshimiwa madiwani, yalianishwa na kumtaka mhandisi wa ujenzi kusimamia na kuhakikisha kazi zote zinaiha katika muda uliopangwa kama mikataba inavyojieleza.



Ghala la chakula kwachaga

Karibu mpenzi msomaji wa Jarida la Handeni yetu awamu ya pili ambapo lengo la jarida letu ni kuhabarisha wananchi juu ya shughuli mbalimbali ambazo zinafanywa na Halmashauri ya Wilaya ya Handeni kwa kipindi cha miezi mitatu mitatu pia ni kuwa nyenzo na daraja la kukuza maendeleo katika Halmashauri. Lengo la Halmashauri ni kuhakikisha kuwa Jarida la Handeni Yetu kupatikana katika kila Ofisi ya Kijiji na Kata ili kuwapa wananchi nafasi ya kusoma na kuelewa namna Halmashauri inavyotekeleza shughuli zake.

Tunaahidi kuendelea kutoa habari na makala ambazo zitakufanya uelewe namna Halmashauri inavyofanya kazi na kutekeleza miradi mbalimbali. Aidha matoleo yajayo yatabeba mambo mengi muhimu ambayo yatakuwa msaada mkubwa kwa wananchi walioko Halmashauri ya Wilaya ya Handeni na Tanzania.

Hapo baadae tunatarajia kuanza kutoa makala maalumu ambazo zitabeba elimu na maarifa yatakayokuwa msaada mkubwa kwa wananchi. Hii itakuwa nafasi nyingine ya kipekee ya kuweza kupata ujuzi pasipo gharama. Ujuzi huu utakuwa katika malengo ambayo yanatekelezwa na Halmashauri.

Aidha tunakaribisha habari na makala mbalimbali kutoka kwenye vijiji na Kata. Makala hizo zinaweza kuelezea jinsi utekelezaji wa miradi na shughuli mbalimbali za maendeleo zilivyofanyika katika kijiji au kata husika.

Asanteni na tunawatakiwa usomaji mwema.



LINATOLEWA NA:

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya wilaya ya Handeni.

S.L.P 355

Handeni, Tanga

Email:ded@handenidc.go.tz

ictsupport@handeni.go.tz



CHF yaja na sera ya Kuku I Tiba mwaka mzima Uk 3



Mkurugenzi aingia Makubaliano na Wakuu wa Shule kuboresha Taaluma Uk 8



Wavamizi msitu wa hifadhi lugala Kitumbi-watakiwa kuondoka maramoja. Uk. 10

Halmashauri ya Wilaya yajipanga kurasimisha na kupima makazi. Uk 7

DIRA (VISION)

Kuwa na jamii iliyoelimika na kuwa na maisha bora.

DHAMIRA (MISSION)

Kuipatia jamii ya Halmashauri ya Wilaya ya Handeni maisha bora kiuchumi kwa kutumia vizuri rasilimali zilizopo kwa kudumisha Utawala Bora ili kuboresha maisha ya jamii

Mfuko wa afya ya jamii CHF yaja na sera ya KUKU 1 tiba mwaka mzima.

Wananchi Wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni wamehamasishwa kujiunga na mfuko wa afya ya jamii CHF ili kupunguza gharama za matibabu na kuwa na uhakika wa kupata matibabu wakati wote pindi huduma ya Afya inapohitajika.

Hayo yalisemwa na Afisa Tawala Wilaya Bi. Upendo Magashi alipokuwa kwenye kampeni ya uhamasishaji wa wananchi kujiunga na kuwa wanachama wa mfuko wa afya ya jamii wa hiari CHF ili kupunguza gharama za matibabu, uliobeba kauli mbiu ya KUKU MMOJA MATIBABU MWAKA MZIMA.

Aliwaeleza wananchi kuwa, kuku mmoja anayegharimu shilingi 10000, anaweza kusaidia kaya moja yenye watu sita kujiunga na mfuko wa Afya ya jamii CHF, ambao watapata matibabu bure kwenye vituo vya Afya kwa ngazi ya Wilaya mwaka mzima. Aliwataka waratibu wa mfuko wa Afya CHF, Wataalamu wa afya, na viongozi mbalimbali kuendelea kutoa elimu na kuwahasishwa wananchi ili kuweza kuwasaidia juu ya umuhimu wa mfuko huo ikiwa ni pamoja na kujibu hoja zao kwa kuzitafutia ufumbuzi.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni Dr. Credianus Mgimba aliwaeleza wananchi kuwa faida mojawapo kubwa ya kujiunga na mfuko wa CHF ni kusaidia upatikanaji wa dawa za kutosha kwenye vituo vya huduma za afya. Wanachama wakiwa wengi itasaidia uwepo wa dawa za kutosha kwani

fedha itakayokusanywa itakuwa nyingi itakayosaidia upatikanaji wa dawa mbalimbali na wanachama wakiwa wachache tatizo la upungufu wa dawa halitakwisha.

Aidha wananchi walielezwa kuwa kuna thamani kubwa sana wakiwa wanachama wa mfuko wa afya ya jamii hasa kwa kaya zisizojiweza kwani husaidia katika kipindi kigumu iwapo mgonjwa atakosa fedha za matibabu, Kwa kutumia kadi ya CHF ataweza kupata matibabu tofauti na kutokuwa mwanachama hali ambayo wakati mwingine hupelekeke hata mtu kupoteza uhai kwani wananchi wengi hawana uwezo wa kujigharamia matibabu. Lengo ni kuhakikisha kila mwananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni anakuwa na uhakika wa huduma ya afya.

Wananchi walielezwa kuwa kwa upande wa wazee ili waweze kuhudumiwa kila kijiji kinapaswa kuchangia laki mbili (200,000) ili iweze kusaidia dhana ya huduma bure ya afya kwa wazee ikiwa ni

upatikanaji wa dawa zinazolenga wazee peke. Mpango huo umepitishwa na baraza la madiwani lililofanyika mwisho mwa mwezi wa kumi na moja hivyo utekelezaji wake unatarajiwa kuanzia Januari mwaka 2017.

Faida za mfuko huo wa Afya ya jamii CHF ni pamoja na kupunguza gharama kama za kufungua faili, kumuona daktari na kununua dawa hali itakayopelekea uhakika wa afya kwa familia nzima.

Hadi kufikia sasa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni ina kaya wanachama 22,532 wa mfuko wa afya ya jamii CHF, Malengo ni kufikia kaya wanachama 26,152 ifikapo June 2017. Uhamasishaji huo ulifanywa kwenye kata saba za Halmashauri ya Wilaya ya Handeni ambapo mwananchi aliyekiunga siku ya uhamasishwaji alitengenezewa na kupeleleka kadi papohapo. Kata hizo ni Segera, Kiva, Kabuku, Komkonga, Kang'ata, Mkata na Kwamsisi.

Kampeni hii inaongozwa na Mhe. Mkuu wa Wilaya na ni endelevu lengo likiwa ni kuwafikia wananchi wote wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni. Awamu ya kwanza imemalizika.



Mwakilishi wa mkuu wa wilaya Bi. Upendo Magashi akihamasisha wananchi wa kata ya komkonga kujiunga na mfuko wa afya ya jamii CHF

HANDENI YETU

Mkuu wa Wilaya ya Handeni Bw. Gondwe azindua zoezi la umezaji wa dawa za kichocho na Minyoo kwenye shule za Msingi

Mkuu wa Wilaya ya Handeni Mh. Godwin Gondwe amezindua zoezi la umezaji dawa za kichocho na minyoo lililoandaliwa na Idara ya Afya, katika shule za msingi zilizopo Halmashauri ya Wilaya ya Handeni. Alizindua umezaji wa dawa hizo katika shule ya msingi ya Mkumburu ikiwa ni kutekelezaji wa mpango wa Taifa wa kudhibiti na kutokomeza magonjwa yaliyokuwa hayapewi ki-paumbele.

Walengwa wa kumeza dawa za kichocho walikua ni wanafunzi wote katika shule za msingi. Wanafunzi wapatao 69550 sawa na asilimia 100% ya wanafunzi wote walikusudiwa kumeza dawa hizo. Aidha watoto walio na umri zaidi ya miaka mitano ambao bado hawajaingia shule waliruhusiwa kumeza dawa hizo.

Serikali ikishirikiana na mdau anayesaidia utekelezaji wa shughuli za mpango huu katika Wilaya ya Handeni shirika la IMA World Health imetoa kiasi cha Tsh. 10,230,000/= ambazo zimegawanywa kwa kila shule. Fedha hizi ni sehemu ya kusaidia mandalizi ya chakula kwa watoto watakaomeza dawa hizo. Walimu na wasimamizi waliandaa maji safi na salama kwa-ajili ya kumeza dawa.

Mkuu wa Wilaya ya Handeni Mh. Godwin Gondwe na Mkurugenzi Mtendaji wa wilaya Bw. William Makufwe waliwataka viongozi wa shule kusimamia na kuhakikisha zoezi hilo linatekelezwa kama

lilivyopangwa na kwa uadilifu wa hali ya juu.



Mh. Gondwe akimpa dawa mmoja wa wanafunzi ikiwa ni ishara ya uzinduzi wa zoezi la umezaji dawa.

Vibakuli zaidi ya 500 na Mbao 914 za mti wa mkarambati zakamatwa

Halmashauri ya Wilaya ya Handeni imefanikiwa kukamata vibakuli zaidi ya 500 vilivyotengenezwa na mti wa mkarambati na mbao 914 aina ya Mkarambati zilizovunwa kinyume cha sheria.

Akitoa taarifa hiyo Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni Bw. William Makufwe alisema Kamati ya mapato ilikamata vibakuli hivyo vyenye soko Nchini Kenya wakati vikitoroshwa kuelekea nchini humo.

Mbao 914 ambazo ni sawa na milioni 24 za Kitanzania zilivunwa kinyume cha sheria kwa kukiuka katazo la kutovuna Miti aina ya Mikarambati ambayo ipo hatarini kutoweka.

Mkurugenzi Mtendaji alisema kuwa watuhumiwa wamekamatwa na

wamefikishwa kwenye vyombo vya sheria na sasa wanasubiri mashauri ya kuzungumzwa mahakamani.



Baadhi ya mbao za mti aina ya mkarambati zilizokamatwa kwa kuvunwa kinyume cha sheria

Mkuu wa Wilaya awataka watumishi na Viongozi ngazi za Vijiji kusimamia Misingi ya Utawala Bora.

Mkuu wa Wilaya ya Handeni Mh. Godwin Gondwe amewataka Maafisa Tarafa, Maafisa Watendaji wa Kata, Watendaji wa Vijiji na Wenyeviti wa Vijiji kusimamia misingi ya utawala bora katika kutimiza majukumu yao ya kuwahudumia wananchi. Aliyazungumza hayo katika kikao kazi alichokitisha siku ijumaa tarehe 28/10/2016.

Mh. Gondwe amewataka viongozi kusimamia rasilimali za umma ikiwemo misitu, ardhi na usimamizi wa suala zima la usafi wa mazingira katika maeneo yao. Pia aliwakumbusha kusikiliza kero za wananchi kuanzia ngazi ya chini ikiwa ni pamoja na kushughulikia malalamiko yao kabla ya kufika ngazi ya Wilaya. Wananchi wanatakiwa kusikilizwa matatizo yao, pale ambapo ngazi za chini zimeshindwa basi ngazi ya Wilaya itashughulika kikamilifu.

Mh. Gondwe amewaeleza Maafisa Watendaji na wenyeviti wa Vijiji kwamba kutokana na mabadiliko hali ya hewa yanayopelekea uhaba wa chakula suala la kulima ekari moja ya muhogo kwa kila kaya ni lazima sio jambo la hiari tena.

Aidha amepiga marufuku kutumia mazao ya chakula katika kutengeneza pombe kwa sababu hali ya chakula kwa sasa katika Wilaya ya Handeni sio nzuri. **“Ni marufuku mazao ya chakula kutumika katika kupikia pombe kwa sababu hatuna chakula cha kutosha”** alisema.

Pia Alitoa tahadhari kwa viongozi na Watendaji kuwa makini na taasisi zisizo za kiserikali (NGO's) zinapokuja kufanya huduma katika maeneo yao, kwani taasisi nyingine zinakuwa hazina dhamira

njema kwa wananchi kwani zimeonekana kufanya mambo ya kitape-li Mfano baadhi yao zimekuwa zikichangisha fedha kwa wananchi bila kufuata utaratibu.



Baadhi ya maafisa Watendaji Kata, Maafisa Tarafa na WenyeViti wa Vijiji waliofika kwenye kikao hicho.

“Viongozi wote na Maafisa Tarafa pale mnapoona kwenye maeneo yenu kuna taasisi zisizo za kiserikali zimekuja na hamuelewi mienendo yao tafadhali naomba mtoe taarifa mapema ili Uongozi wa Wilaya uweze kushughulikia mapema” alisema.

Aidha Mkuu wa Wilaya ya Handeni aliwataka wataalamu wa Kitengo cha misitu kusaidia kuainisha hifadhi za misitu kwa ngazi ya Serikali kuu, Halmashauri na Vijiji ili wananchi waweze kuyatambua na kwamba watu wote waliovamia maeneo ya hifadhi waondoke wenyewe kwa hiari yao kabla ya Serikali kuu na Halmashauri ya Wilaya haijawaondoa kwa nguvu.

Alisisitiza kwamba suala la kulinda maeneo ya hifadhi kama vile misitu, vyanzo vya maji na maeneo yaliyohifadhiwa sio la hiari.

Aliitaka Halmashauri kuripoti

pindi uharibifu wa maeneo hayo unapofanyika.

Aidha Alipiga marufuku pia watoto chini ya umri wa miaka 18 kuchunga ng'ombe hasa siku za shule

na kuwaripoti watu wanaoharibu miundombinu ya maji.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya ya Handeni Bw. William Makufwe alisema kutakua na zoezi kupanda miti laki 6 kwa msimu unaokuja wa mvua ambapo kila kaya itatakiwa kupanda miche ya miti kumi (10) ambayo watalazimika kuitunza ili iweze kukua.

Mkurugenzi mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni alimuhakikishia Mkuu wa Wilaya kwamba atasimamia utekelezaji wa maelekezo yote aliyoyatoa ikiwemo utawala bora utakao husisha usomwaji wa mapato na matumizi katika vijiji vyote, utunzaji miti, hifadhi ya misitu, ulinzi wa miundombinu na vyanzo vya maji.

HANDENI YETU

Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI Bw. Sulemani Jaffo amewaasa watumishi wa umma na Viongozi kuacha kufanya kazi kwa mazoea.



Mh. Waziri Jaffo Akizungumza na Viongozi na Watumishi kwenye ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni

Serikali imewataka maafisa elimu kupanga muda wa kusikiliza kero za walimu na kuzitafutia ufumbuzi ili kuongeza morali ya walimu kufundisha. Agizo hilo lilitolewa na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Suleman Said Jaffo alipokuwa akiongea na walimu wa shule ya sekondari Segera iliyopo wilayani Handeni, wakati wa ziara ya kiserikali Wilayani Handeni na Mkoa wa Tanga.

Mhe. Jaffo alisema kuwa wapo baadhi ya Maafisa elimu ambao wanajifanya kuwa ni Miungu watu linapokuja suala la kusikiliza na kutatua kero za walimu. Waziri Jaffo alisema. alisema **“Wapo walimu wanaotembea umbali mrefu kufuata huduma makao makuu ya Halmashauri kwa wakubwa wao mara nyingi wameshindwa kutatuliwa kero zao hali inayopelekea usumbufu, Kuanzia leo 24/11/2016 napiga marufuku tabia hiyo”**.

Aliongeza msisitizo kuwa Maafisa elimu wapo kwa lengo la kuwasikiliza walimu na kuwasaidia kutatua kero zao ili waweze kujikita katika ufundishaji wa wanafunzi. Alisema kuwa walimu ni watu muhimu sana nchini ila wamekuwa wakikatishwa tamaa na utendaji wa baadhi ya maafisa elimu. Aliongeza kuwa kero kubwa ya walimu ni kutokupanda madaraja kwa wakati na kutopata stahiki zao ikiwa ni pamoja na posho za likizo, uhamisho na madai mengine.

Wakati huohuo, Naibu Waziri aliiagiza Halmashauri ya Wilaya ya Handeni kukamilisha miradi yote ya SEDP-II ambayo haijakamilika kuhakikisha inakamilika kabla au ifikapo tarehe 20/12/2016. Alisema kuwa katika kusimamia miradi hiyo na miradi ya maendeleo kwa ujumla kila mtu lazima atimize wajibu wake na kuhakikisha fedha iliyotengwa na kutolewa inatumika vizuri na thamani yake kuonekana kwa muda mrefu (value for money). Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI aliwataka Maafisa

utumishi kusimamia vizuri haki za watumishi ili kuwawezesha watumishi wote kufanya kazi kwa moyo na kuwaondolea msongo wa mawazo usio wa lazima. **“Maafisa utumishi wakifanya kazi zao kwa weledi na kutimiza wajibu wao, Halmashauri haitakuwa na malalamiko kutoka kwa watumishi kitu ambacho kitaoongeze ufanisi katika utendaji wao”**. Vilevile, aliwataka kutambua michango ya watumishi bora na wanaojituma kufanya kazi kwa juhudi na maarifa na kuwepo kwa utaratibu wa kuwapa pongezi na motisha (acknowledgement).

Aidha aliwaeleza waweka Hazina kuhakikisha wanatimiza wajibu wao kwa kufuat sheria, taratibu na kanuni za Halmashauri kwani kufanikiwa au kutofanikiwa kwa malengo ya Halmashauri kunachangiwa kwa kiasi kikubwa kwa utendaji kazi wa waweka Hazina wa Halmashauri. **“Mwekahazina atayeshindwa kutimiza wajibu wake atapisha nafasi hiyo kwa mtu mwingine ambaye ataweza kusimamia kwa ufanisi”** alisema.

Pia aliwaagiza Wakurugenzi wa Halmashauri ya Mji Bw. Kennedy Haule na Bw. William Makufwe Mkurugenzi wa Handeni Vijijini kuweka malengo ya utendaji kazi kwa kutumia mfumo wa Opras kwa kila Mkuu wa Idara na kitengo na kuhakikisha wanafuatilia kwa karibu utendaji kazi wa watumishi hao, ili kutambua kwa kiasi gani malengo hayo yamekamilishwa. Wametakiwa kuhakikisha UK 7

pia wanakuza vipaji vya watumishi kwa kutumia elimu na taaluma walizonazo ipasavyo ili kuendeleza Halmashauri.

Wakurugenzi wametakiwa kuhakikisha pia watumishi wa idara ya maendeleo ya jamii wanatumika ipasavyo katika kuhudumia jamii ikiwa ni pamoja na kuhakikisha fedha za miradi ya vikundi vya vijana na kinamama zinatolewa na kutumiwa kama ilivyokusudiwa.

Mwisho Naibu Waziri aliwashukuru watumishi na kuwaomba wapendane kwani upendo baina ya watumishi ni chachu ya maendeleo kwamba kila mtumishi afanye maju kumu yake kwa kukuza thamamani ya na kutoa ushirikiano kwa

viongozi wetu hasa wabunge. Aliwakumbusha watumizi kufanya kazi kama ajira kwani wanapata mishahara, kucha alama (legacy) na kufanya kazi kama ibada kwa kuwatumikia wananchi.

Aidha, Aliwataka Waheshimiwa Madiwani kufanya maamuzi sahihi pindi linapofika suala la kufanya maamuzi kwa manufaa ya wananchi na sio kunufaisha Viongozi wachache au kikundi cha watu. Hasa upatikanaji wa eneo la kujenga ofisi za Halmashauri zilizo gawanywa ili kuondoa gharama zisizo za lazima za ulipaji fidia wa maeneo.

Mkuu wa wilaya ya Handeni Mh. Godwin Gondwe aliahidi kusimamia utekelezaji wa maagizo yote yaliyotolewa na Naibu Waziri kwa

karibu na ukamilifu wake kwa dharti .

Naye Mbunge wa Jimbo la Handeni Mjini, Mhe. Omary Kigoda alitoa shukrani kwa ziara ya Naibu Waziri, ambapo alitumia fursa hiyo kumuomba Naibu Waziri kusaidia upatikanaji wa watumishi wa sekta ya afya kutokana na uhaba mkubwa wa watumishi wa kada hiyo hali inayoyofisha huduma kwa jamii. Alisema kwamba watumishi waliopo ni 25% ya watumishi wanaohitajika hivyo upungufu ni mkubwa.

Naibu Waziri Jafo alifanya ziara ya siku moja Wilayani Handeni ambapo pamoja na mambo mengine aliongea na watumishi wa wilaya hiyo.

Halmashauri ya Wilaya Handeni yajipanga kupima na kurasimisha Makazi.

Halmashauri ya Wilaya ya Handeni kupitia Idara ya ardhi, misitu na maliasili imejipanga kupima na kurasimisha makazi kwenye miji ya Mkata, Kabuku na Seger/Michugwani.

Kaimu Mkuu wa Idara ya adhi, Misitu na Maliasili akiwasilisha tarifa ya urasimishaji makazi na upima wa maeneo ambayo bado hayaenda kutasaidia wananchi na serikali kunufaika kwa kuzuia ujenzi wa makazi holela na kuwa na mji uliopangwa kitaalamu.

Alieleza kuwa zoezi hilo litasaidia kumiliki ardhi kisheria kupitia hati za muda wa miaka 33 zitakazowasaidia wananchi kutumia kama dhamana katika taasisi za kifedha ili waweze kujikwamua kiuchumi.

Kurasimisha na kupima maeneo kutasaidia kutenga maeneo muhim

u ya huduma za jamii na miundombinu ya barabara ambayo ni muhimu katika kuboresha maisha ya Binadamu. Aidha itapunguza pia Migogoro ya ardhi inayosababishwa na wananchi kumiliki ardhi isiyopimwa na iliyopimwa bila kufuata taratibu na sheria ya ardhi.

Halmashauri itaongeza mapato, serikali za vijiji na Serikali kuu kupitia makusanyo ya kodi mbalimbali za ardhi, kodi ya majengo (property tax) na gharama za maandalizi ya hati mara baada ya upimaji kukamilika.

Aidha utekelezaji wa zoezi hili umepangwa kuwa shirikishi ambapo makadirio ya gharama za kuandaa mchoro wa mipango miji pamoja na upimaji kwa viwanja 500 inakadiriwa kugharimu Tsh. 75,000,000/= . Kuandaa mchoro wa mipango miji Tsh.25,000,000/=

kila mwananchi atachangia Tsh.50,000/=

Gharama za upimaji Tsh. 50,000,000 ambapo kila mwannachi atachangia 100,000/= na kumilikishwa ardhi kisheria kupitia hati za muda mrefu yaani miaka 33 atachangia 200,000, Hivyo jumla ya gharama za mipango miji, upimaji, mchoro wamipango miji na umilikishwaji(kupewa hati miliki) kila mwananchi atachangia jumla Tsh.350,000/=.

Viongozi ngazi ya Vitongoji katika maeneo hayo wataelimishwa juu ya mpango huo ambapo uchangishwaji wa fedha za utekelezaji wa zoezi hilo utafanywa na makao makuu ya Halmshauri badala ya kusimamiwa na serikali za vijiji. Hii itasaidia kuongeza imani kwa wananchi kwamba Serikali imekusudia kutoa huduma hii.

HANDENI YETU

Ofisi ya Mkurugenzi kupitia Idara ya Elimu Msingi na Sekondari imejipanga kuongeza kiwango cha ufaulu 2017

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni Bw. William Makufwe amengia makubaliano ya kimaandishi kati na waalimu wakuu, wakuu wa shule za Sekondari na waratibu Elimu kata jinsi ya kusimamia ufundishaji na kuinua taaluma katika shule na Kata hadi kufikia asilimia 76% mwaka 2017.

Akizungumza kwenye mkutano uliojumuishwa wataalamu wote wa Elimu kuanzia ngazi ya Msingi hadi Sekondari, Mkurugenzi Mtendaji aliwaeleza kuwa, Lengo ni kubaini shule zenye upungufu mkubwawa waalimu na kurekebisha ikama ya waalimu kufikia walimu 7 kwa kila shule ya Msingi yenye darasa la kwanza hadi la saba na idadi ya wanafunzi 350.

Ofisi ya Mkurugenzi kupitia Idara ya Elimu Msingi na Sekondari zitawajibika kufuatilia ufundishaji shuleni, kusikiliza changamoto zinazowakabili walimu na kutoa ushauri mara moja kila robo ya mwaka.

Aidha walielezwa kuimarisha Elimu ya kujitegemea ambapo kila shule ya Msingi na Sekondari itapaswa kulima Ekari 2 za mahindi na ekari moja ya muhogo na mazao mengine ili ziweze kuzalisha chakula cha mchana kwa wanafunzi na walimu.

Walikubaliana pia kuwasimamia waalimu waweze kutoa mazoezi ya kutosha kwa wanafunzi na majaribio ya juma na mwezi na kuendesha mitihani ya utimilifu (mock) ngazi ya Wilaya kwa madarasa la nne na la tano ngazi ya Msingi na kidato ch II & IV ngazi ya Sekondari.

Mkurugenzi Mtendaji aliwataka Maafisa watendaji Kata na Vijiji kusimamia mahudhurio ya wanafunzi shuleni kwa kuzitaka Serikali za Vijiji na Kata

kuchukua Hatua mapema dhidi ya wazazi/ walezi ili kudhibiti utoro wa wanafunzi. Aliwataka kutoa adhabu kwa wazazi na walezi watakaosababisha utoro huo itakapobidi.

Idara ya Elimu Msingi na Sekondari walielezwa kuhakikisha wanajengea uwezo kamati na bodi za shule katika vikao vya robo ya kwanza na pili ili zitambue nafasi yao katika kuinua maendeleo ya Taaluma katika shule zao.

walikubaliana kuwa agenda ya

Msingi na Sekondari kujadiliwa katika mikutano ya kamati za maendeleo ya Vijiji/Kata na kuibuka na mikakati ya kuinua kiwango cha taaluma katika Kata.

Mwisho aliwataka Viongozi wote ngazi ya Vijiji chini ya Maafisa Elimu Wilaya kuendelea kuelimisha jamii kuhusu tafsiri sahihi ya waraka wa Elimu bila malipo ili wachangie chakula cha mchana na kushiriki katika shughuli za kuboreshaji wa miundombinu ya shule.



wanafunzi wa shule ya Msingi Mkumburu wakipata maelezo kutoka kwa waalimu wao

Mashimo 13,232 ya kutupia taka yamechimbwa katika kata 9 za Halmashauri ya Wilaya ya Handeni.

Katika kutekeleza agizo la Mh. Rais la usafi wa mazingira wa kila mwisho wa mwezi Halmashauri ya Wilaya ya Handeni chini ya kitengo cha mazingira na udhibiti wa taka ngumu kimeendelea kusimamia na kuhakikisha kata 21 zilizopo zinatekeleza pamoja na makao makuu ya Halmashauri.

Kitengo kimefanya ufuatiliaji wa uchimbaji wa mashimo ya kutupia takataka

kwenye kata 10 ambapo jumla ya mashimo 13,232 ya kutupia taka yamechimbwa ambapo, fedha kutoka mradi wa kampeni ya Taifa ya usafi wa mazingira NSC imetumika utekelezaji wa zoezi hilo.

Kitengo kimeendelea kuhamasisa wananchi katika kata zote 21 kutumia maji safi na salama hii ikiwa ni kuchemsha maji kabla ya kuyatumia.

HANDENI YETU

Maadhimisho ya siku ya Maadili na Haki za binadamu yafanyika kiwilaya wilayani Handeni

Wananchi Wilayani Handeni wametakiwa kufuata maadili katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku ili kujihahakikishia huduma bora za jamii.

Kauli hiyo ilitolewa na Mkuu wa Wilaya ya Handeni Mh. Godwin Gondwe alipokuwa akisikiliza kero za wananchi wa Kata ya Segera iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Handeni jana katika maadhimisho ya siku ya Maadili na Haki za Binadamu Kiwilaya yaliyoandaliwa na taasisi ya kuzuia na kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU).

Mh. Gondwe alisema “**Maadili ni imani njema, sehemu yoyote yenye maadili haki za binadamu hufuatwa, hakuna ardhi itakayouzwwa kiholela, wagonjwa watati biwa vizuri kwenye vituo vya afya, wageni wataingia kwenye maeneo yetu kwa kufuata taratibu za nchi na shughuli zote zitafanyika kwa misingi ya Haki**”. Aidha aliwataka watumishi wa umma na wananchi kwa ujumla kufuata sheria, taratibu na kanuni pasipo kujali wala kubagua rangi au cheo cha mtu yeyote. Alisema kuwa Rushwa ni adui wa haki na kuwataka kuikataa kwa kauli na vitendo.

Wakati huohuo Mkuu wa Wilaya ya Handeni alivunja baraza la Ardhi la Kata kwa kulalamikiwa na wananchi kutotekeleza maajukumu yeke na kuwaagiza TAKUKURU Wilaya ya Handeni kulichunguza hadi ifikapo mwishoni mwa mwezi Januari 2017, na mapungufu yoyote-



Mh. Gondwe akisikiliza kero za mmoja wa wananchi katika siku ya maadhimisho yaliyofanyika Michungwani.

yatakayobainika basi hatua za kisheria zichukue mkondo wake maramoja. Vilevile aliwaaagiza Maafisa Watendaji wa Kata na Vijiji kusimamisha shughuli zote za kilimo zinazofanywa kwenye msitu wa hifadhi ya kijiji

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni Bw. William Makufwe aliwataka Maafisa Watendaji na wenyevitwa wa Vijiji kusimamia miradi yote ya maendeleo kwa maadili na uadilifu kutokana na dhamana kubwa waliyonayo kwenye maeneo yao ya kiutawala. Vilevile aliwataka kusoma tarifa za mapato na matumizi na kuwa tayari kujibu hoja za wananchi kuhusu taarifa za mapato na matumizi. “Mtendaji atakayehindwa kusoma taarifa za mapato na matumizi atakua amejiondoa mwenyewe kwenye nafasi yake” Alisema Makufwe.

Mkuu wa TAKUKURU Wilaya Bi. Esta Mulima, alisema TAKUKURU itaendelea kupambana na Rushwa kikamilifu na kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu madhara ya Rushwa.

Aliwataka wananchi kufichua vitendo vya rushwa vinapotokea au dalili za vitendo hivyo ili hatua ziweze kuchukuliwa.

Maadhimisho ya siku ya Maadili na Haki za Binadamu hufanyika kila tarehe 10 Disemba Kitaifa, na Wilayani hapa yalifanyika tarehe 8 Disemba kutokana na Muingiliano wa Majukumu yakiiongozwa na kauli mbiu isemayo

“kujenga na kukuza maadili, haki za binadamu, uwajibikaji, utawala bora na Mapambano dhidi ya Rushwa”.



Mkurugenzi Mtendaji Bw. William Makufwe akihutubia wananchi kwenye siku ya maadhimisho.

HANDENI YETU

Wavamizi wa Msitu wa Lugala kata ya Kitumbi watakiwa kuondoka mara moja.

Mkuu wa Wilaya ya Handeni Mh. Godwin Gondwe amefanya ziara ya kusuluhisha mgogoro wa Wakulima na wafugaji na uvamizi wa msitu wa hifadhi wa lugala kijiji cha Kitumbi.

Katika ziara hiyo Mkuu wa Wilaya aliambatana na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni Bw. William Makufwe pamoja na wataalamu wa Halmashauri. Bw. Gondwe amewapa siku 30 kuanzia tarehe 18/11/2016 wakulima na wafugaji waliovamia msitu wa hifadhi wa Lugala kuondoka kabla sheria haijachukua mkondo wake.

Amewaeleza wananchi kuwa kila eneo lina utaratibu wake na kijiji cha kitumbi ni miongoni mwa vijiji vyenye mapango wa matumizi bora ya ardhi na kwamba kila eneo litumike kulingana na mpango bora ulivyoainishwa kwa kufuata taratibu na sio vinginevyo.

Amepiga marufuku tabia kwa baadhi ya Viongozi wa Vijiji kukaribisha wageni hususani wafugaji bila kufuata utaratibu, mwenye kukiuka hilo sheria kali itachukuliwa dhidi yake. Ameyatamka hayo baada ya kubaini kuwa baadhi ya viongozi wa Vijiji wanahusika moja kwa moja kwa kuwakaribisha wafugaji katika maeneo yao kiholela bila kufuata utaratibu kwa maslahi binafsi hali inayopelekea migogoro ya ardhi kwa wananchi baadae.

Amewaeleza kuwa mfugaji yeyote haruhusiwi kuingia kwenye eneo la Handeni bila kuwa na kibali kutoka kwa Mkuu wa Wilaya au

mkurugenzi. Mwenye kukiuka agizo hilo hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake kama mhalifu mwingine yeyote kwani hakuna mtu yeyote ambaye yupo juu ya sheria.

Aidha, amepiga marufuku ulishaji wa mifugo kwenye mashamba ya watu hata kama hakuna mazao na kwamba mtu yeyote atakayebainika kufanya hivyo akamatwe na kupeleka polisi. Aliwaomba wananchi kutoa ushirikiano wa kuwaripoti watu na viongozi wanaouza ardhi kiholela kwani wao wanawafahamu zaidi.

Wakati huohuo Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni Bw. William Makufwe amemsimamisha kazi Mtendaji wa Kijiji cha Kitumbi Bw. Omary Salehe kwa utovu wa nidhamu kwa kutosoma mapato na matumizi kwa wananchi kwa muda wa miezi 11. Mkurugenzi amewaeleza wanakijiji kwamba Mkaguzi wa ndani atakwenda kukagua taarifa za mapato na matumizi za miezi sita iliyopita ili kupata ripoti kamili wakati mtendaji huyo akipisha uchunguzi.



Viongozi wakisikiliza kero za wananchi kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika kata ya Kitumbi.

Mkurugenzi Mtendaji aliwataka Watendaji wa Vijiji kuhakikisha wanasoma taarifa za mapato na matumizi kila robo ya mwaka inapokwisha kwani kwa kutofanya hivyo kutapelekea viongozi hao kuondolewa kwenye nafasi zao. Ameyazungumza hayo baada ya wanakijiji wa kitumbi kulalamika kutosomewa mapato na matumizi kwa muda wa miezi 11.

Aidha aliwaeleza wananchi kuwa suala la maendeleo ni jukumu la kila mwananchi na kwamba katika ujenzi wa shule na zahanati wananchi wanatakiwa kuonesha nia na uhitaji kwa kuanza kujenga majengo na Serikali itasaidia katika hatua za mwisho yaani rent na upauaji.

Mkuu wa Wilaya aliwashukuru wanakijiji cha Kitumbi kwa uvumilivu wao, aliwataka kuendelea kudemisha amani na kuwaahidi kuwa suala la tatizo la maji linakwenda kuisha kwani mikakati ya kuikomboha Handeni na janga la maji imeanza utekelezaji wake.

HANDENI YETU

HABARI KATIKA PICHA



Afisa Utumishi Wilaya Bw.Noel Abel akieleza maana ya Utawala bora kwenye kikao kilichofanyika Anglikana.



Mwanasheria Wa Wilaya Bw. Amani Mangesho aki-zungumza na Viongozi kufuata sheria za uuzaji wa ardhi na namna ya kuingia Mikataba, Anglikana



Mganga Mkuu wa Wilaya Bw. Credeneus Mgimba Akihamasisha wananchi kujiunga na CHF ili kupunguza upungufu wa dawa.



Mwenyekiti kamati ya Elimu, Afya na Mji mh. Joel Mabula akihamasisha wananchi kujiunga na CHF kwenye kata ya Komkonga.



Ujenzi wa vyumba nane vya matundu ya choo cha wasichana , mradi uliotembelewa na kamati ya Fedha,Uongozi na Mipango shule ya Sekondari Mkata



kamati ya Fedha Uchumi na Mipango ikipata maelezo mfupi ya ujenzi wa madarasa 4 shule ya sekondari ndolwa wakati wa ziara ya ukaguzi

HANDENI YETU

HABARI KATIKA PICHA



Naibu Waziri Bw. Jafo mwenye suti nyeusi akiwa na baadhi ya walimu wa shule ya Sekondari Segera.



Naibu Waziri Bw. Jafo akisaini kitabu cha mahudhurio shule ya Sekondari Segera kushoto ni Mkurugenzi, kulia ni Mkuu wa Wilaya.



Ujenzi wa vyoo bora vya wanafunzi wa shule ya Sekondari Segera ukiwa katika hatua za mwisho za ukamilishaji, katika kuhakikisha Usafi wa vyoo kuepuka maradhi.



Baadhi ya watumishi walioshiriki kikao cha Naibu Waziri Jaffo alipokuwa akizungumza na watumishi wa Umma.



Ukaguzi wa nyumba ya waalimu 6 inayojengwa shule ya Sekondari Ndolwa, ikiwa ni kuhakikisha mkandarasi analiza kazi ndani ya muda uliopangwa.



Kamati ya Fedha, Uchumi na Mipango ikiendelea na ukaguzi wa ujenzi wa barabara ya komkonga-luiye-mzungu katika kuangalia kiwango na ubora wa barabara hiyo.